

**OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NC**  
**FOMU YA HAKI ZA MTEJA (DSS-6237)**

Jina la Mtoa Huduma za Wakimbizi: \_\_\_\_\_

Kama wateja wa Mtoa Huduma huyu wa Wakimbizi, una haki fulani ambazo zinajumuisha haki ya:

- kushiriki katika uundaji wa mpango wa huduma na kujulishwa kuhusu matarajio ya kila mhusika kwa lugha unayoelewa.
- kuundiwa mpango wa huduma usio na masharti mengi/rahisi unaofaa.
- kutarajia kwamba hakuna maelezo yanayokuhusu utakayoombwa yatakayotolewa kwa wengine bila idhini yako iliyoandikwa.
- kufikia faili yako ya mteja ukiomba kwa madhumuni ya ukaguzi.
- kulindwa kwa utambulisho wako kwenye ripoti, takwimu, mihtasari ya kesi, filamu au nyenzo zingine zozote za habari zilizochapishwa bila idhini yako iliyoandikwa.
- kutobaguliwa kwa sababu ya asili, dini, rangi, umri, utaifa, ulemavu, jinsia, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi au hali ya ndoa.
- kutoshiriki katika maonyesho ya umma, kutakiwa kutoa taarifa za umma za kushukuru shirika au kushiriki katika shughuli za utafiti.
- kutonyanyaswa kijiinsia na/au dhuluma yoyote ya kimwili, kihisia au kimatamshi.
- kukataa huduma yoyote inayotolewa na mtoa huduma za wakimbizi. Hata hivyo, kukataa huduma hizi kunaweza kusababisha kukomeshwa kwa misaada na athari zingine zitakazoelezwa na mfanyakazi. Huduma zinaweza kukomeshwa; (1) ukihama katika eneo linalohudumiwa na mtoa huduma au (2) ukikataa kushirikiana na mtoa huduma za wakimbizi.
- kuonyesha kutoridhika na huduma zinazotolewa na kuwasilisha malalamiko. Ikiwa una matatizo, wasiliana na:

1 - Mtoa Huduma za Jamii/Mfanyakazi wa Shirika \_\_\_\_\_ Nambari ya Simu \_\_\_\_\_

2 - Msimamizi wa Wafanyakazi \_\_\_\_\_

3 - Meneja wa Eneo: \_\_\_\_\_

4 - Mkurugenzi wa Shirika la Wakimbizi \_\_\_\_\_

5 - Mratibu wa Huduma za Wakimbizi wa Jimbo la NC: \_\_\_\_\_

Unapaswa kujadili maswali yoyote kuhusu haki hizi na mtoa huduma wako wa jamii.

Saini ya Mfanyakazi wa Shirika \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Tafadhali tia saini fomu hii baada ya kumaliza kuisoma au kufafanuliwa kwako.

Saini ya Mteja \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Ninathibitisha kuwa mteja anaelewa haki zilizobainishwa hapo juu.

Saini ya Mkalimani \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Fomu halisi ya Haki za Mteja inapaswa kuwekwa kwenye faili ya mteja na mteja apewe nakala yake.

**Maagizo ya Kujaza**  
***Fomu ya Haki za Mteja ya Ofisi ya Wakimbizi ya Jimbo la NC (DSS-6237)***

Huduma ya Wakimbizi Mtoa Huduma:	Weka jina la shirika ambalo linatoa huduma kwa mteja.
Mtoa huduma za jamii/ Mfanyakazi wa Shirika:	Weka jina la mtoa huduma za jamii au mfanyakazi wa shirika aliyekabidhiwa mteja na nambari zao za simu.
Msimamizi wa Kesi:	Weka jina la msimamizi wa kesi ambaye anamsimamia moja kwa moja mtoa huduma za jamii aliyekabidhiwa mteja. Ikiwa haitumiki, andika Haitumiki katika nafasi iliyowekwa.
Meneja wa Eneo:	Weka jina la meneja wa eneo ambaye anasimamia moja kwa moja ofisi inayompa mteja huduma. Ikiwa haitumiki, andika Haitumiki katika nafasi iliyowekwa.
Mkurugenzi wa Shirika la Wakimbizi:	Weka jina la mkurugenzi wa shirika la wakimbizi ambalo linampa mteja huduma.
Mratibu wa Huduma za Wakimbizi wa Jimbo la NC:	Weka jina la mratibu wa huduma za wakimbizi wa jimbo la North Carolina kwenye nafasi iliyowekwa.
Saini ya Mfanyakazi wa Shirika:	Mfanyakazi wa shirika anayejaza fomu hii lazima atie saini na tarehe kwenye fomu katika nafasi iliyotolewa.
Saini ya Mteja:	Mteja lazima atie saini na aandike tarehe tarehe katika nafasi zilizotolewa.
Mkalimani:	Mkalimani lazima atie saini na tarehe ili kuthibitisha kwamba mteja anaelewa haki zilizobainishwa kwenye fomu hii. Ikiwa hakuna mkalimani aliyehitajika, tafadhali andika Haitumiki.

**Fomu halisi ya Haki za Mteja inapaswa kuwekwa kwenye rekodi za mteja na mteja apewe nakala yake.**